

# Kumfuata Yesu huko KIRIBATI

## KUTANA NA SCOTT!



### Kuhusu Scott

**UMRI:** miaka 8

**KUTOKA:** Tarawa, Kiribati

**LUGHA:** Kiribati na Kiingereza

**MALENGO NA NDOTO:** Kuwa daktari

**FAMILIA:** Mama na Scott



## Jinsi Gani Scott Anamfuata Yesu

Scott ni mtiifu na mkarimu. Anapenda kuwa mfano mzuri, hasa kwa binamu yake mdogo. Yeye ni rafiki mwema sana kwa binamu yake kiasi kwamba siku zote anamwita mdogo wake. Scott anasali kila usiku na kila asubuhi. Kila siku anapenda kwenda kwenye shughuli za Kanisa, na anapenda jioni ya nyumbani. Yeye anapenda kuwasaidia wengine pia. Anataka kuwasaidia wengine kwa sababu anahisi vizuri anapofanya hivyo. "Kuwasaidia watu wengine kunanifanya niwe na furaha," anasema.

VIELELEZO NA AMANDA YOSHIDA



### Wewe Unaweza Kumfuata Yesu Pia!

Kuna njia nyingi za kumfuata Yesu. Je, unaweza kufanya nini ili kumfuata Yeye? Andika na utuelezee!

## Mapendeleo ya Scott

**HADITHI YA MAANDIKO:** Wakati Yesu Kristo alipozaliwa



**MAHALI:** Kwenye nyumba ya mababu zake



**TUNDA NA MBOGA:** Matufaha, brokoli



**SOMO SHULENI:** Kiingereza



**RANGI:** Bluu